

Hizi ni siri ambazo hazitakuwa siri tena kwako, kwa sababu dakika chache zijazo ninakwenda kuzifunua mbele ya macho yako.

Ninakufunulia uzijue ili uzitumie vizuri kuimarisha mahusiano yako na kupunguza migogoro hasa kwenye kuwasiliana na mwanaume wako.

Ukizifahamu leo tulia kama vile huzijui, huku ukimchora tu huyo mwanaume wako.

muachie uwanja wa kujiona yeye ndiyo yeye amekuweza hadi mwisho, kumbe wewe unamalengo bora kuliko yake nayo ni kutunza mahusiano yenu yazidi kuwa ya maelewano zaidi na amani.

Yaani natamani ajione kama anapita kwenye njia aliyoibuni yeye kumbe wewe ndiye uliyetengeneza bila yeye kujua, nahitaji ucheze na mwanaume wako kama mwanao.

Mwanamke mwenye ufahamu na hekima huijenga nyumba yake na mwanamke mpumbavu huibomoa nyumba yake yeye mwenyewe.

Kuwa mwanamke mtulivu lakini kumbe ni mkorofi mno, jifanye kama mtumishi na kumbe wewe ndiye boss.

Mfanye mwanaume aweanafanya kile unachotaka pasipo yeye kujua kwa kutumia mbinu hizi tu nitakazo kwenda kukufundisha kwenye kitabu hiki.

Mwanaume akikushinda kuishi naye uwe ni uzembe wako tu, lakini karibia vitu vyote utavikuta humu.

Mfanye mwanaume wako kuwa mwanaume, niamini mimi utafurahia maisha mno, utaona atakavyokufanyia vitu vya kipekee sana kwenye maisha yako.